Jarida la UQAB

Toleo 10
Novemba 2017 Miladi
Safar 1439 Hijriya

Wala Msiwe Katika Washirikina Katika Wale Walioitenga Dini Yao

Watoto Katika Uislamu

Athari Mbaya Itokanayo na Kugawanya Elimu Kuwa ya Kidini au Kidunia

Pindi Akili Inapokuwa Mtunzi wa Sheria

Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi -Halaqa 6

SWALI / JAWABU: Kilicho Nyuma ya Kura ya Maoni Juu ya Kulitenga Eneo la Kurdistan



# Demokrasia Nchini Kenya Ni Mvutano Kati ya Amerika na Uingereza

# Demokrasia Nchini Kenya Ni Mvutano Kati ya Amerika na Uingereza ilhali Chaguzi Ni Njia Tu ya Kufikia Utawala na Kuthibitisha Uhalali Wake

Kenya kama ilivyo nchi nyengine yoyote ya kidemokrasia ulimwenguni huchukua nidhamu yake ya utawala ya demokrasia kutoka kwa mfumo batili wa kirasilimali. Urasilimali ni mfumo ambao aqeedah yake ni ilmaniy -kutenganisha dini na serikali/maisha. Hivyo basi, huipa demokrasia kupitia wanademokrasia ukiritimba katika kudhibiti/kutunga sheria za mambo ya kimaisha kwa msingi wa akili zao finyu na kwa kipimo makhsusi cha vitendo kilicho jengwa juu ya manufaa/maslahi. Kwa hivyo, ili kuielewa hali iliyoko sasa nchini Kenya tunalazimika kuregelea historia yake, ambayo ni kuwa Kenya ni koloni ya Uingereza na mpaka leo iko chini ya mashiko yake kikamilifu. Kuthibitisha hili, tutaangazia siasa na uchumi wake ambazo ndizo nguzo kuu kulingana na mfumo wa kirasilimali ili kufafanua wamiliki wake halisi. Kenya inategemea kikamilifu makampuni ya Kiingereza kuimarisha uchumi wake, ambayo baadhi yake yakiwa ni Unilever, BAT, benki ya Standard Chartered, Safaricom, Base Titanium, Tullow, Bunson Travel Service, STA Travel Kenya, Scott Travel Group nk.

Kisiasa; kihakika Kenya imeundwa ili kusalia kuwa koloni ya Uingereza mpaka leo, lakini; katika waraka 'katiba' ikatangazwa kuwa huru mnamo 1963 na kupewa mipaka yake na bendera yake ili kuwaziba macho watu kuwa iko huru. Baada ya Vita vya Pili vya Dunia Uingereza ilipata hasara nyingi na kutokana na hayo ikaunda mpango wa kupunguza matumizi yake ya kiuchumi kwa kutawala na kusimamia moja kwa moja koloni zake ili kuinua nchi yake. Katika mpango wake, iliamuliwa kuwa koloni zote za Uingereza zisimamiwe kupitia kwa vibaraka wao watiifu na Jomo Kenyatta alichaguliwa baada ya kuyeyushwa na maadili ya kimagharibi kwa muda mrefu. Kwanza alichaguliwa kama Waziri Mkuu kisha kuwa raisi wa kwanza wa Kenya. Jomo Kenyatta alichaguliwa si kwa sababu anatoka katika kabila kubwa la Wakikuyu nchini Kenya, lakini; kwa sababu ya kuwa tayari kwake kuitikia na kutenda kwa mujibu wa maagizo ya mabwana wa kikoloni wa Kiingereza na hili lilithibitishwa alipo anzisha mashambulizi makali dhidi ya Wakikuyu wenzake ambao hawaku jisalimisha chini ya utawala wake. Kwa kuwa waliuona utawala huo kuwa mabadiliko tu ya sura na rangi, lakini; sera za ubaguzi ziliendelea hususan katika kufikia afisi za juu, vyeo na ugavi wa ardhi zenye rutuba kufanywa kwa mataraji pekee, na wale walio kuwa karibu na Kenyatta, wandani wake wanaojumuisha Waingereza kwa gharama ya wenyeji maskota hadi wa leo!

Kama njia ya kuidhinisha kikamilifu utawala wa Kenyatta wenye kunyenyekea kwa Uingereza bwana mkoloni, ni wakati wa kifo chake mnamo 22 Agosti 1978 ambapo Uingereza ilimteua Bruce Roy Douglas McKenzie kuongoza matayarisho ya mazishi yake. Muundo wa mazishi ulipambwa katika hali iliyo shabihiana na mazishi ya mwenda zake Waziri Mkuu wa Uingereza Winston Churchill. Wawakilishi wakuu wa Kiingereza akiwemo mwana wa malkia Charles, mrithi wa ufalme wa Uingereza, alihudhuria mazishi yake.

Daniel Arap Moi akachaguliwa kama kibaraka mpya wa ukoloni wa Kiingereza kwa sharti kwamba aendeleza dori aliyo cheza Jomo Kenyatta. Moi aliitumikia Kenya bila ya wasiwasi wowote kwa sababu alifurahia usaidizi wa mabwana zake wa Kiingereza kwa muda wa miaka 24. Katika utawala wote wa Moi alishuhudia kuibuka kwa sura ya utawala wa Kiamerika ukipambana na utawala wa mabwana zake wa kikoloni wa Kiingereza barani Afrika, ikiwemo Kenya.

Mnamo miaka ya thamanini Amerika ikafaulu kushawishi na kukusanya pamoja waliokuwa vibaraka wa Uingereza kama Jaramogi Oginga Odinga na mwanawe Raila Odinga ambao walikuwa wakilingania 'demokrasia na vyama vingi' kuandaa mapinduzi ambayo hayakufaulu, lakini; yakatoa fursa zaidi kupanua athari ya Amerika nchini Kenya. Watu walipoteza maisha katika jaribio la mapinduzi na Raila Odinga akatiwa nguvuni, kutuhumiwa kwa kosa la uhaini na kuwekwa kizuizini pasi na kuhukumiwa kwa miaka sita. Raila aliachiliwa mnamo Februari 1988 na kukamatwa tena mnamo Septemba 1988 kwa kuwa kibaraka wa Amerika kwa 'kuunga mkono vuguvugu la kutetea demokrasia na haki za kibinadamu'. Huku Raila akiwa gerezani Amerika ilifaulu pakubwa kuathiri na kumvuta mkikuyu mkubwa, mwenye usemi katika jamii na aliyekuwa kibaraka wa Uingereza, Kenneth Matiba. Kwa hivyo Raila alipoachiliwa kutoka gerezani mnamo 12 Juni 1989, alifungwa tena mnamo 5 Julai 1990 pamoja na Kenneth Matiba na aliyekuwa Meya wa Nairobi Charles Rubia kwa kulingania mfumo wa vyama vingi na watetezi wa haki za kibinadamu. Raila hatimaye aliachiliwa huru mnamo 21 Juni 1991, na mnamo Oktoba, alikimbilia hifadhi nchini Norway kwa usaidizi wa rafiki yake na kibaraka wa shirika la ujasusi la Kiamerika FBI hali zilipoonyesha kuwa serikali ya Kenya inapanga kumuua bila ya mafanikio.

Huku Raila akiwa ng'ambo, Amerika ikafaulu kuanzisha kuundwa kwa chama cha FORD chini ya uongozi wa Jaramogi Oginga na Kenneth Matiba, ambacho baadaye kilisambaratika kutokana na kuchakachuliwa na Moi na kuzaliwa FORD-Kenya kilicho ongozwa na Jaramogi Oginga Odinga, na FORD-Asili kilicho ongozwa na Kenneth Matiba. Kenneth Matiba akafaulu kushindana dhidi ya Daniel Arap Moi katika uchaguzi wa 1992 lakini; akanyimwa ushindi kwa sababu hakuwa katika kambi ya Uingereza. Badala yake, Moi akatangazwa mshindi!

Mnamo 1994 baada ya babake Raila

*Endelea Uk..3*



Email: uqab@hizb.or.ke

kufariki FORD-Kenya ikawa chini ya uongozi wa Kijana Wamalwa kikaragosi wa Uingereza. Raila akaamua kupambana na Wamalwa kung'ang'ania uongozi wa chama na uchaguzi kukumbwa na kashfa na Raila kukihama na kujiunga na NDP kilicho undwa na Stephen Wilfred Omondi Oludhe. Raila kama kibaraka wa Amerika kutoka katika jamii ya Waluo iliyo ya tatu kwa ukubwa nchini akajaribu kugombea uraisi kwa mara ya kwanza mnamo 1997 na kuibuka wa tatu, lakini; alihifadhi kiti chake kama mbunge wa Langata. Kutokana na ushauri na baraka kutoka kwa bwana wake Amerika, Raila akaamua kumuunga mkono Moi kikaragosi wa Uingereza na hasimu wake mkuu, na kuingia katika muungano wa kisiasa kati ya chama chake, NDP na KANU kuunda kile kilichoitwa 'KANU Mpya' iliyopelekea Raila kuteuliwa kuwa waziri wa kawi kuanzia mnamo Juni 2001 mpaka 2002. Lengo kuu la Amerika lilikuwa kupatiliza fursa iliyo iva kwa 'miito ya mageuzi' nchini Kenya ili Raila aweze kumrithi Moi. Hili lilithibitishwa kwa uchaguzi uliofuatiwa wa KANU baadaye mwaka huo; Raila akachaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa chama (akamuondoa J.J. Kamotho).

Lakushangaza ni kuwa Amerika ilishindwa kwa ujanja na Uingereza mnamo 2002 wakati Moi alipo muidhinisha Uhuru Kenyatta mwana wa mtawala kibaraka wa kwanza wa Uingereza nchini Kenya; kuwa mgombea uraisi katika uchaguzi mkuu wa 2002. Hili lilimfanya Raila kuhama 'KANU Mpya' na kuasisi vuguvugu la Rainbow pamoja na wanachama wengine waasi wa KANU waliohisi chaguo la Moi kuwa baya. Kisha Raila akalibadilisha vuguvugu la Rainbow na kuunda chama cha LDP. Kisha LDP ikaungana na chama cha DP kilichoongozwa na Mwai Kibaki, NPK kilichoongozwa na Charity Ngilu na FORD-Kenya kilichoongozwa na Michael Kijana Wamalwa wakaunda muungano wa NARC ulio husisha vyama 15 vya kisiasa lakini hivi vinne vikawa ndio wahusika wakuu.

Wakati huu Amerika ikapiga mahesabu yake kuwa kwa kuwa nchini Kenya ina Raila pekee kama kikaragosi wao muaminifu na waliosalia wote ni watiifu kwa Uingereza wanaomzunguka kibaraka wao. Walimshauri Raila kumuunga mkono Mwai Kibaki kikaragosi wa Uingereza, lakini; kwa masharti ya mkataba wa maelewano (MOU) kuwa NARC itakapo chukua uongozi, ataunda cheo cha Waziri Mkuu kwa Raila Odinga na kuteua nusu ya baraza lake la mawaziri kutoka upande wa LDP. NARC ikafika uongozini kwa ushindi mkubwa sana wa asilimia 61% dhidi ya KANU 31% hivyo basi Uhuru Kenyatta kukubali kushindwa na Mwai Kibaki kuapishwa afisini mnamo 30 Disemba 2002 kama raisi wa tatu wa Kenya. Mara moja Kibaki akakataa kuheshimu MOU na hili likamaanisha kuwa Uingereza iliishinda kwa ujanja Amerika kwa mara ya pili. Lakini; bado Raila akabakia katika serikali ya Kibaki, lakini; akipanga njama dhidi yake. Moja ya njama hizo ilikuwa ni kuanzisha kura ya maamuzi ya katiba iliyolenga kupunguza nguvu za raisi.

Mnamo 2005, Raila akafanya kampeni dhidi ya Mwai Kibaki huku akiongoza wenzake kuasi serikali iliyo kuwa upande wa kuipigia kura ya 'Ndio' na Raila akilingania kura ya 'La'. Mnamo 21 Novemba 2005, timu iliyoongozwa na Raila ikaishinda timu ya Kibaki kwa asilimia 57% na 43% mtawalia katika matokeo ya kura ya maamuzi. Hivyo basi, Amerika ikaishinda Uingereza katika kura hiyo ya maamuzi. Mwai Kibaki alisonga mbele na kumuadhibu Raila na ambaye ni tishio kwa serikali yake na maslahi ya bwana wake mkoloni. Akalifuta kazi baraza zima la mawaziri mnamo 23 Novemba 2005. Lilipoundwa upya wiki mbili baadaye, Raila na wanachama wote wa LDP waliachwa nje! Amerika ikamshauri Raila kupatiliza fursa ya kufaulu katika kampeni iliyo muwezesha kushinda kura ya maamuzi kusajili chama kipya cha upinzani, vuguvugu la chungwa ODM-Kenya; kwa kuwa chungwa ilikuwa ndiyo alama ya kura ya 'La' katika kura ya maamuzi ya katiba. Mnamo Agosti 2007 chama hicho kilichakachuliwa na watiifu wa Uingereza walio pelekea kukigawanya kuwa vyama viwili huku Raila akichukua ODM na Kalonzo Musyoka akichukua ODM-Kenya.

Mnamo 2007, Raila akafanya jaribio lake la pili la kugombea uchaguzi wa uraisi. Wakati huu Amerika ilikwenda katika uchaguzi mkuu huku vichwa vyao vikiwa juu kwa kuzingatia kuwa Raila alikuwa ni kiongozi wa upinzani na alikuwa ameshinda kura ya maamuzi hivi punde. Licha ya hayo, Raila alinyimwa ushindi katika uchaguzi mkuu wa 27 Disemba 2007 na Mwai Kibaki kutangazwa mshindi mnamo 30 Disemba 2007. Raila alipinga ushindi huu na kutoa wito kwa jamii ya kimataifa kuingilia kati; huku Kalonzo Musyoka kinara wa chama cha ODM-K akimkumbatia na kumuunga mkono Kibaki na moja kwa moja kuzawadiwa cheo cha Makamu wa Raisi.

Kufuatia miezi miwili ya ghasia, iliyopelekea maelfu ya watu kuuwawa, kunajisiwa, kuwa wakimbizi na uharibifu mkubwa kuonekana katika mali na uchumi kwa jumla. Makubaliano kati ya Raila na Kibaki, yalitoa mwanya wa ugavi wa mamlaka na kuundwa kwa cheo cha Waziri Mkuu, yalitiwa saini mnamo Februari 2008. Ilisimamiwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa UM Kofi Annan 'kikaragosi wa Amerika '; yaliungwa mkono na Jendayi Frazer – Waziri Msaidizi wa Kigeni wa Masuala ya Afrika kama mpatanishi pamoja na ziara ya Condoleeza Rice mnamo 17 Februari 2007. Raila Odinga aliapishwa kama Waziri Mkuu, pamoja na ugavi wa mamlaka katika baraza la mawaziri, mnamo 17 Aprili 2008. Hii ilikuwa mara ya kwanza kwa utawala wa Amerika kuhisi kupata kitu cha kihakika katika mamlaka chini Kenya. Huku Uingereza ikitumia fursa ya hali iliyoko kumuinua Uhuru Kenyatta kwa kumchagua kuwa Naibu Waziri Mkuu na mrithi wa Mwai Kibaki katika uchaguzi mkuu ujao wa 2013.

Kama sehemu ya kuandaa mazingira muwafaka baina ya Uingereza na Amerika kulingania katiba mpya kukaibuka kwa 'kusemekana' kuwa ghasia zilitokana na changamoto zinazo lighubika taifa tangu uhuru,

*Endelea Uk.4*

hivyo basi mageuzi msingi na vifungu vilitungwa na kura ya maamuzi kupendekezwa. Lakushangaza ni kuwa mwanzoni Uhuru mtiifu mkuu wa Uingereza wakati huo hakuwa upande wa kura ya 'Ndio' na pia alihofia ikiwa atashirikiana na Raila muonekano wake wa kitaifa utafinikwa na ule wa Raila ambaye ni mshindani wake mkuu katika uchaguzi mkuu ujao. Raila alikuwa akiunga mkono katiba, itakayo anzisha serikali za kaunti zinazo shabihiana na muundo wa Kiamerika na mapendekezo mengineyo kutoka kwa bwana wake Amerika ambayo yalipitishwa kupitia ziara ya Joe Biden mnamo 7 – 9 Juni 2010.

Mnamo 2010, Uingereza alimshauri 'Uhuru' kushikamana na kambi ya 'Ndio' na wao 'Uingereza' kuunga mkono hasimu wake mkuu ambaye sasa amegeuka kuwa rafiki William Ruto katika kambi ya 'La'. Hivyo basi, hatimaye wangeutumia msimamo wa Ruto ambaye angeibuka kama kiongozi shupavu wa kambi ya 'La' na kiongozi wa chama cha URP kwa manufaa ya Uhuru Kenyatta. Kambi ya 'Ndio' ilishinda kwa asilimia 68.6% huku kiongozi wa kambi ya 'La' William Samoe Ruto (wakati huo Waziri wa Elimu) akikubali kushindwa. Hii ilithibitisha kufaulu kwa karata ya Uingereza ambayo baadaye iliitumia Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (ICC) kuwaunganisha Uhuru Kenyatta pamoja na William Samoe Ruto wanaotoka katika maeneo yaliyo na wapiga kura wengi eneo la Kati na Bonde la Ufa la Kenya kwa mwito wa kilaghai wa 'Amani na Maridhiano'. Hivyo basi, idadi ya wapiga kura maeneo hayo ikiongezewa kutoka kwa makabila mengine yanayo egemea kwao ilikuwa ni jambo la uhakika kwao kushinda uchaguzi mkuu wa 2013, ambao daima hutegemea hadithi ya ukabila.

Mnamo 2013, Raila alikuwa na uhakika wa kumrithi Kibaki kwa matarajio kuwa Uhuru Kenyatta na William Ruto hawatakuwa kizingiti kwake kwa cheo uraisi, lakini; kwa mara nyengine tena, Uingereza ikaishinda kwa ujanja Amerika katika siasa za urithi za Kenya koloni yake. kwa kutumia hadithi ya Mahakama ya ICC kuyaunganisha maeneo mawili haya ya Kati na Bonde la Ufa nyuma ya watu hawa wawili. Walipigia debe hadithi ya kirongo ya udharura wa amani iliyo maanisha bila ya viongozi wawili hawa kufikia ngazi ya utawala hakutakuwa na amani wala maridhiano nchini Kenya ikizingatiwa matukio ya baada ya uchaguzi wa 2007 ambayo wengi wa waathiriwa ni jamii kutoka maeneo/makabila haya. Amerika ilipogundua hili ikashindwa kwa ujanja Raila akaanzisha kampeni ya kuunda muungano wa vyama unaojulikana kama CORD. CORD ilihusisha chama cha Raila cha ODM, chama cha Wiper cha Kalonzo Musyoka (kilicho kuwa ODM-K) na chama cha Moses Wetangula cha Ford Kenya (FK) kuwania uraisi na Raila akawa mgombea na Kalonzo Musyoka kama mgombea mwenza wake. CORD ilikuwa ikikabiliana na muungano wa Jubilee (Uhuru Kenyatta – TNA), William Ruto (URP), Charity Ngilu (NARC) na Najib Balala -Republican Congress (RC)). Jaribio la tatu la Raila kugombea uraisi lilikuwa mnamo 4 Machi 2013, lakini; Uhuru Kenyatta akatangazwa mshindi mnamo 9 Machi 2013. hivyo basi, Raila akenda kotini, iliyokuwa chini ya mashiko ya Uingereza, ikahalalisha ushindi wa Uhuru Kenyatta.

Mnamo 2017, Amerika bila ya kuwa na mtu mwengine badala katika upande wa utiifu wakaamua kwa mara ya nne mfululizo kumuunga mkono Raila kwa uchaguzi wa uraisi. Ambapo walimunnga mkono Raila kuunda muungano wa NASA. NASA ilijumuisha ODM ya Raila, chama cha Wiper cha Kalonzo Musyoka, chama cha FORD-Kenya cha Moses Wetangula, chama cha ANC cha Musalia Mudavadi, chama cha NARC cha Charity Ngilu, chama cha PPK cha Moses Akaranga, chama cha CCU cha Wavinya Ndeti, na chama cha Muungano (MP). Mgombea uraisi wa NASA akawa Raila na Kalonzo mgombea mwenza wake wakikabiliana na chama cha Jubilee kikiongozwa na Uhuru Kenyatta kama mgombea wake wa uraisi na William Ruto mgombea mwenza wake.

Baada ya uchaguzi wa mnamo 8 Agosti 2017, kwa mara nyengine tena Uhuru Kenyatta akatangazwa mshindi mnamo 11 Agosti 2017. Raila kwa mara nyengine akapinga matokeo katika Mahakama ya Upeo ya Kenya na mara hii ushindi wa Uhuru Kenyatta ukabatilishwa mnamo 1 Septemba 2017. Hii ilimpatia Raila fursa ya kugombea kwa mara ya tano kushiriki marudio ya uchaguzi mnamo 26 Oktoba, 2017. Badala yake akajiondoa akitaja kuwa sababu zilizo pelekea kubatilishwa kwa uchaguzi bado hazijatatuliwa. Kwa hivyo Raila akaitisha mkutano bustani ya Uhuru Park Nairobi mnamo 25 Oktoba 2017 na kusema NASA imebadilishwa na kuwa 'Vuguvugu la Kitaifa la Uasi' kwa lengo la kushinikiza mageuzi nchini Kenya

Huo hapo juu ni ufafanuzi wa kina, lakini; tunaufupisha kuwa ni 'mvutano kati ya Marekani na Uingereza kupitia vikaragosi wao nchini Kenya'. Mwishowe raia wakiwemo 'wasomi na wasiokuwa wasomi' ni sehemu tu ya kitendawili cha kisiasa. Ni hadaa tu ya 'wahusika wakuu au mibabe ya kikabila' wanao pigania maslahi yao, lakini; damu na jasho lao ndizo hutumika kama ngazi za kuwapandisha 'Vibaraka' mamlakani na hususan kushiriki kwao katika chaguzi ni kuhalalisha na kuidhinisha serikali ambazo ziko pale kuhudumia wamagharibi na sio wao. **Kila damu inapomwagwa zaidi ndipo nafasi kubwa ya mazungumzo inapatikana mbele ya 'meza ya mamlaka'** katika kila upande wa kisiasa.**Muda uliobakia wa Marekani ni sasa** kwa sababu hatima yao bila Raila ni giza kwao.

**Enyi Waislamu na Wanadamu** ulimwenguni kote epukeni demokrasia, inaleta maangamivu kwa kila inapopitia na kwa kila anayeikumbatia.

**Ali Nassoro**
**Mwanachama wa Hizb ut Tahrir Kenya**

Offisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 01 / 1439 AH | Jumanne, 04 Safar 1439 Hijria | 24/10/2017 Miladi

# Wala Msiwe Katika Washirikina Katika Wale Walioitenga Dini Yao Na Wakawa Makundi Makundi Kila Kikundi Kinafurahia Kilicho Nacho

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Hatua ya mahakama ya juu kuamuru marudio ya uchaguzi Oktoba 26, 2017 imezusha fukuto la kisiasa nchini. Baada ya kuubatilisha uchaguzi wa mwezi Agosti 2017, kumeshuhudiwa vuta ni kuvute juu ya usimamizi wa uchaguzi mpya baina ya mirengo miwili ya kisiasa (Jubilee na Nasa). Jubilee inaonekana kutokuwa na wasiwasi juu ya tume ya IEBC; imezama katika kampeni za kuwataka watu kushiriki katika uchaguzi. Kinara wa Nasa Raila Odinga ambaye aliyejitoa kwenye uchaguzi amekuwa akiwasihi wafuasi wake kususia kura kwa msingi kuwa IEBC kattu haiwezi kuendesha uchaguzi wa huru na haki. Huku haya yakijiri, wabunge wa Jubilee ambao ndio wengi bungeni tayari wamependekeza marekebisho ya kanuni za kiuchaguzi yanayolenga kuzuia mahakama kubatilisha matokeo ya kura. Aidha, merekebisho hayo ni kuwa mgombezi yoyote atakayejitoa kwenye marudio ya uchaguzi basi aliyebaki atangazwe mshindi moja kwa moja.

**Harakati ya Kiislamu ya Hizb ut Tahrir Kenya** ingependa kusema yafuatayo:

Malumbano haya baina ya wanasiasa hayafaidishi mwananchi wa kawaida kwa hali yoyote ile isipokuwa kumzidishia kero baada ya kero. Haya ni mashindano baina yao juu ya kufikia uwezo wa kisiasa na hata wa kiuchumi kwa lengo la kupata maslahi tu baina yao wala sio kwa maslahi ya raia walala hoi. Vinara wa mirengo yote hii sio wageni machoni mwa raia bali wote wemehudumu katika serikali zilizopita na wakapora mabilioni ya pesa za umma. Hakuna miongoni mwao walio na nia kweli ya kutatulia raia matatizo msingi licha ya Kenya kuwa moja wapo ya nchi duniani zilizo na pengo kubwa baina ya matajiri na masikini.

Mzozo huu unadhihirisha kushindwa kwa mfumo wa kibepari na siasa yake ya kikoloni ya Kidemokrasia. Isitoshe, hali hii imefichua kasoro kubwa ya asasi kuu za tawala za Kidemokrasia ikiwemo katiba na mahakama. Wanademokrasia baada ya kudharau sharia za Mwenyezi Mungu hujitungia katiba kisha wenyewe huzidharau huku kila mmoja akiifasiri atakavyo ili kuridhisha upande wa kisiasa! Na mgongano baina ya Bunge na Mahakama kama ilivyodhihirika pale wabunge wa mrengo wa Jubilee kupendeza marekebisho ya kanuni za uchaguzi za kudhoofisha uwezo wa mahakama! Kisha pasina na hata chembe ya haya wanademokrasia hudai kuwa mahakama ni huru hazifai kuingiliwa! La hatari zaidi, ni mahakama ya juu kutofautiana katika uamuzi wa kesi huku majaji wakitoa hukumu zinazogongana! Licha ya aibu na fedheha zote hizi bado mataifa ya kimagharibi kupitia mabalozi wao kwa jeuri na kiburi chao hawasiti kuingilia masuala ya ndani ya Kenya na kujifanya wanahuruma nayo ilhali ukoloni wao mambo leo ikiwemo Demokrasia yao ndio chanzo cha majanga yote kote.

Masikitiko ni kuwaona wasomi na wadadisi nchini Kenya hadi sasa bado wanaendelea kutekwa na urongo wa Demokrasia. Na lakutia machungu zaidi ni kuwaona viongozi wa Kiislamu wakijigawa kimakundi kila kundi la masheikh likisherehekea na kufurahia urongo wa Demokrasia na wanasiasa wake.

Mwisho twaonya jamii ya Kenya na hasa ya Kiislamu kutekwa na miito ya chuki ya wanasiasa ya kugawanya raia kwa lengo la kufikia maslahi yao ya Kisiasa. Huu ni wakati mwafaka wa jamii ya Kiislamu kuonyesha uwezo wa Uislamu na mafundisho yake ya kutatua matatizo yanayokumba Kenya bali dunia nzima.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari**
**Hizb ut-Tahrir Kenya**

# Watoto Katika Uislamu



Uislamu ni dini iliyoteremshwa na Allah (swt) kwa wanadamu wote, kila sehemu, na kila zama. Kwa ajili hiyo, Uislamu uko wazi kwa kila mtu na unatilia maanani umuhimu wa heshima, haki, na majukumu. Aya za Quran na Hadith sahih za Mtume Muhammad (saw) zina jumuisha haki na majukumu kutoka Allah (swt) kwa wanadamu. Kamwe hayategemei matamanio na matakwa ya wanadamu, wake kwa waume, hivyo basi hayabadiliki. Haki hizi za kipekee zilizo tajwa na Uislamu hujumuisha pia haki za watoto. Haki za watoto hazikudhaminiwa na wazazi wao, jamii, serikali au hata mashirika yasiyo kuwa ya kiserikali. Bali Allah (swt) mwenyewe ndiye Aliyedhamini haki hizi za watoto.

Uislamu umeweka mpangilio wa kisheria, na mkusanyiko wa maadili, yaliyoundwa kulinda haki za mtu binafsi ikiwemo haki ya kuishi ndani ya mujtama salama. Kwa watoto, usalama una umuhimu mkubwa. Haki za watoto zinaanza hata kabla ya kuzaliwa; kihakika huanza kabla ya utunzi wa mimba. Qur'an na hadith sahih za Mtume Muhammad (saw) zinaweka wazi kuwa watu wawili hawapaswi kuingia katika ndoa kiholela. Mazingatio na matayarisho makubwa ni muhimu kabla mume na mke kujitolea kukaa pamoja na kwa familia ambayo itatokamana na fungamano lao. Kutoka kwa Abu Hurayrah amesema, Mtume (saw) amesema:

**روى أبو داود والنسائي عن أبي هريرة رضي الله عنه: قال النبي صلى الله عليه وسلم: تنكح المرأة لأربع لمالها ولحسبها ولجمالها ولدينها فاظفر بذات الدين تربت يداك**

"Mwanamke huolewa kwa ajili ya mambo manne: kwa ajili ya mali yake, nasaba yake, urembo wake, na dini yake, chagua dhati ya dini mikono yako itajifunga (kutokamana na fitna)." (Abu Dawud)

Ikiwa mume na mke wote wamejitolea maisha yao kumuabudu na kurimdhisha Muumba wao, basi wanapaswa kutambua kwamba haki za watoto wowote watakao kuwa nao kiasili zimedhaminiwa. Kumuabudu Allah (swt) humaanisha kutii maamrisho yake; na miongoni mwa maamrisho yake ni kuhifadhi haki za mtoto. Kupitia ndoa kinyume na uhusiano haramu wa zinaa wanandoa huwa tayari wameanza safari ya kuhifadhi haki za watoto wao wa siku za usoni ikiwa ni haki ya mtoto kuifahamu nasaba yake.

Mimba ya mtoto pindi inapotungwa, ina haki ya kuishi. Qur'an imeweka wazi kuwa maisha ya kiumbe ni matukufu. Kamwe hairuhusiwi

*Endelea Uk..7*

kuavya 'kutoa' mimba kwa hofu ya kutoweza kusimamia mahitaji ya kifedha ya mtoto au mtoto wa pili. Allah (swt) pekee ndiye mwenye kuruzuku na kuhuisha katika maisha. Allah (swt) asema:

وَلا تَقْتُلُوا أَوْلادَكُمْ مِنْ إِمْلاقٍ نَحْنُ نَرْزُقُكُمْ وَإِيَّاهُمْ

...**wala musiwauwe watoto wenu kwa sababu ya umasikini. Sisi tunawaruzuku nyinyi na wao**.[Al-An'aam: 151]

Mtu anapofanya uamuzi wa kuavya 'kutoa' mimba ni muhimu kukumbuka kwamba kupata mtoto ni baraka kutoka kwa Allah (swt) na baraka zote mfano wa hii hazina budi kupokewa kwa furaha na shukrani. Kuna watu wengi ulimwenguni leo ambao hawana uwezo wa kupata watoto, hivyo basi ikiwa Allah (swt) ataibariki familia kwa mtoto, inatakiwa iwe ni sababu ya sherehe na furaha. Licha ya hayo watoto sio vinyago wala mali tu za kumilikiwa; kupata mtoto huja na jukumu kubwa nyuma yake.

Qur'an na hadith sahih za Mtume Muhammad (saw), zinazungumza waziwazi kuhusu jukumu la malezi ya mtoto. Ni wajib juu ya Waumini kuwalea na kuwajali watoto wao kwa kuwakuza kuwa watu wenye maadili mema na uchaji Mwenyezi Mungu. Kujenga utambuzi kwao kuwa wao ni miongoni mwa wanadamu wenye thamani kwa watu jumla na hususan kwa familia zao. Kupuuza jukumu hili hupelekea kumtoa mtu katika njia ya wema na kumueka mbali na radhi za Allah (swt):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا قُوا أَنفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ عَلَيْهَا مَلَائِكَةٌ غِلَاظٌ شِدَادٌ لَّا يَعْصُونَ اللَّهَ مَا أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ

**Enyi mlioamini! Ziokoeni nafsi zenu na za jamaa zenu na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Juu ya Moto huo kuna Malaika wakali wenye nguvu, hawamuasi Allah kwa anayo waamrisha, na wanatenda wanayo amrishwa.** [At-Tahriim: 6]

Kutoka kwa Abdullah ibn 'Umar amesema: nimemskia Mtume (saw) akisema:

عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ يَقُولُ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ...: وَالرَّجُلُ رَاعٍ فِي أَهْلِهِ وَهُوَ مَسْئُولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ، وَالْمَرْأَةُ رَاعِيَةٌ فِي بَيْتِ زَوْجِهَا وَمَسْئُولَةٌ عَنْ رَعِيَّتِهَا...

**...na mume ni mchungaji kwa watu wa familia yake na ataulizwa kutokana na anao wachunga, na mke ni mchungaji katika nyumba ya mumewe na ataulizwa juu ya anavyo vichunga** (Bukhari na Muslim)

Kuwajali na kuwalea watoto katika njia inayostahili ni jukumu kwa wazazi na daima si jambo rahisi hususan leo chini ya mfumo batili wa kimagharibi wa kirasilimali pamoja na maadili yake yaliyooza kama fikra za uhuru. Kihakika, Allah (swt) anatukumbusha katika Qur'an kuwa watoto huenda wakawa mtihani mkubwa kwa wazazi wao. Ushindi na majaribio katika maisha ni katika mitihani na watoto ni sehemu yake. Wanaweza kuleta furaha na huzuni kubwa vile vile. Allah (swt) asema:

إِنَّمَا أَمْوَالُكُمْ وَأَوْلَادُكُمْ فِتْنَةٌ ۚ وَاللَّهُ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ

**Hakika mali zenu na watoto wenu ni fitna. Na kwa Allah upo ujira mkubwa (Pepo).** [At-Taghaabun: 15]

Kufuata mafundisho ya Uislamu humwezesha Muumini kukabiliana na matukio yote ya kimaisha ikiwemo mitihani, fitna na ushindi. Nasaha sahihi ya Kiislamu juu ya malezi na kuwakuza watoto inajumuisha nyanja zote za maisha. Ni nasaha tukufu kama ulivyo Uislamu wenyewe. Kuimarika upande wa kimwili, hisia na kiroho vyote vina umuhimu sawa. Ni muhimu kutilia maanani kuwa Uislamu daima umejumuisha haki za watoto. Mtazamo wa Uislamu kuhusu utoto unaeleza kuwa ni kipindi cha kipekee katika uhai wa mtu. Hii ni kinyume na mtazamo wa mfumo wa batil wa kimagharibi ambapo fikra ya utoto haikuzungumziwa mpaka katika karne ya 16. Sio kuwa wamagharibi hawakuwa na watoto au vijana bali waliwachukulia kuwa watu wazima wachanga walio na mahitajio na matakwa sawa na watu wazima wapevu.

Katika historia yote ya Uislamu na katika fasihi ya Kiislamu haki na majukumu yanayo husiana na watoto yamefafanuliwa kwa uwazi. Wazazi, familia, na jamii wana majukumu maalumu juu ya watoto. Mengi yao yakiwa ya wajib, na siku ya Qiyama, Allah (swt) atawauliza watu wazima kuhusu jinsi walivyo watendea watoto wao.

Watoto wetu ni amana tuliyopewa na Allah (swt). Hivyo basi, kwa muktadha huu, wanatakiwa wapewe lishe bora, wavishwe vizuri, waongozwe kiroho na wafuatiliwe kwa makini katika fahamu zao (Aqliyya) na utendaji wao (Nafsiyyah). Wanapaswa kukuzwa kwa thaqafa imara ya Kiislamu ili kuzalisha ndani yao utambulisho 'shakhsiyya' wa Kiislamu wenye uwezo wa kuubeba Uislamu kama fikra na njia, na kuwatayarisha katika njia hiyo, kwa jukumu kubwa la ubebaji ulinganizi wa kuregesha tena maisha kamili ya Kiislamu kupitia kusimamisha tena dola ya Khilafah kwa Njia ya Utume.

**Masoud Salim Mazrui**
**Mwanachama wa Hizb ut Tahrir Kenya**



# Athari Mbaya Itokanayo na Kugawanya Elimu Kuwa ya Kidini au Kidunia

Ni dhahiri kwa mwenye macho na anayefuatilizia kwa umakinifu kuona athari mbaya kwa elimu ya Kiislamu itokanayo na kupigwa mafungu kwa elimu kuwa ya kidini na kidunia ndani ya mfumo batil wa kirasilimali. Mtazamo huu umezaliwa kutokamana na msingi wa Aqeeda potofu ya kutenganisha dini na maisha. Hivyo basi, elimu ya kidunia haina mahusiano yoyote na dini bali iko kwa lengo la kumpa mwanadamu mwelekeo wa kimaisha na mwelekeo huu kamwe haupaswi kuwa maregeleo yake ni wahyi.

Athari kuu inayojitokeza wazi wazi ni kudharauliwa ile inayodaiwa kuwa elimu ya kidini; yaani fungamano la kiroho la kumtambua Allah (swt) na utambuzi wa jinsi ya kutekeleza ibada kwake. Mfumo batil wa Urasilimali umewafunga macho baadhi miongoni mwa Waislamu kuthamini elimu hiyo ya 'kidunia' kutokana na kule kuambatanishwa moja kwa moja na suala la riziki au ajira. Hii imepelekea mpaka wazazi kupuuzilia mbali suala la kuwapa thaqafa sahihi watoto wao na badala yake kuwafanyia bidii watoto wao kufaulu katika elimu ya kisekula ili wawe watu maarufu maishani. Maustadhi na makhatibu wameoneka kutokuwa kiigizo kwa wanafunzi kwa kuonekana watu waliopitwa na wakati na wenye kuishi maisha duni!

Dalili ya haya ni kauli mbiu ambayo husikika mara kwa mara wanafunzi wakihimizwa na wazazi au walimu mashuleni kutia bidii ya juu masomoni ili kuweza kujipatia kazi nzuri kama udaktari, uhandisi, urubani na kadhalika. Shule zimeongeza mpaka muda wa ziada wa masomo; hadi majira ya usiku, kiasi ya kuwafanya wanafunzi kutopata muda wa kuisoma na kuifahamu dini yao tukufu ya Uislamu na kuurudia kama mfumo utokao kwa Allah (swt) ili kutatua matatizo yanayoukumba ulimwengu.

Uislamu huitazama elimu kuwa jumla kutoka kwa Allah (swt) kwa ajili ya kumnufaisha mwanadamu katika maisha yake hapa duniani na kesho akhera. Na hufanya utafutaji wa elimu kuwa faradhi kwa kila Muislamu sawa sawa iwe faradhi ya lazima (Fardh 'Ayn) kama kutafuta elimu ya thaqafa ya Kiislamu katika kumjua Allah (swt) na utekelezaji ibada kwake, au faradhi ya kutoshelezana (Fardh Kifayah) kama kutafuta elimu ya fani, sayansi na sanaa kama udaktari na uhandishi, kiasi ya kuwa ikiwa faradhi mbili hizi hazikutekelezwa, ummah watakuwa katika madhambi. Kutoka kwa Anas ibn Malik asema: kutoka kwa Mtume (saw) amesema:

عن أنس بْنِ مَالِكٍ قَالَ :عن النبيِّ صلَّى اللهُ عليهِ وسلَّم أنه قال)) :طَلَبُ العِلْمِ فَرِيْضَةٌ عَلَىْ كُلِّ مُسْلِمٍ )) . رواه ابن ماجه

**Kutafuta elimu ni faradhi (ya lazima au ya kutoshelezana) kwa kila Muislamu.** [Ibn Majah]

Jinsi hii ya usomeshaji elimu katika Uislamu huondoa ile dhana kwa mwanafunzi kuwa baadhi ya mambo hayana ufumbuzi wake katika Uislamu ila kwengineko, na badala yake kujenga kanaa katika nafsi yake kuwa Uislamu ni mfumo kamili unao muongoza na kumpa mwanadamu elimu kamilifu katika kila nyanja za maisha yake; kuanzia namna ya kutekeleza swala na saumu mpaka katika udaktari na uhandisi n.k.

Ama katika suala la elimu, riziki au ajira; Uislamu, huyatazama kuwa mambo mawili tofauti wala hayafai kuchanganywa au moja kufanywa kuwa sharti ya jengine. Chini ya serikali ya Kiislamu ya Khilafah, msingi wa siasa ya elimu ni Aqeedah ya Kiislamu. Nayo ni kumfahamisha mwanafunzi kuwa lengo kuu la kusoma ni kutafuta radhi za Allah (swt) kwa kunufaika nayo na kuwanufaisha wengine. Na riziki kama mojawapo ya masuala ya Aqeedah, haiko mikononi mwetu bali iko katika mzunguko unaomtawala mwanadamu. Kiwango cha elimu alichonacho mtu sicho kinacho dhamini riziki kwake bali Allah (swt) humpa amtakaye pasi na hisabu au pasi na kuzingatia kiwango cha elimu alichonacho.

Ama lengo la siasa ya elimu katika Uislamu chini ya dola ya Khilafah litakuwa kuwasomesha wanafunzi elimu yenye maana kwao katika mambo ya kimaisha badala ya kuwabebesha mzigo wa masomo mengi usiowaletea faida yoyote maishani mwao baada ya kuhitimu masomoni. Hatimaye serikali kubuni fursa muafaka zitakazo wawezesha raia wake kujikimu kimaisha ima kama wafanyikazi wa ummah au wa kibinafsi katika nyanja zote pasi na kubagua katika upande wa kiroho au wa kimada.

**Imad Mohammad**



Email: uqab@hizb.or.ke

# Pindi Akili Inapokuwa Mtunzi wa Sheria, Taharuki Hutawala

Miaka mitano iliyopita, Profesa Miroslav Djordjevic, mtaalamu wa upasuaji na urekebishaji viungo vya uzazi anayeongoza duniani, alipokea mgonjwa katika kliniki yake ya Belgrade. Alikuwa ni mgonjwa aliyejibadilisha jinsia yake aliyefanyiwa upasuaji katika kliniki nyengine kuondoa uume wake – na tangu wakati huo amebadili mawazo yake. Hiyo ilikuwa mara ya kwanza kwa Djordjevic kuagizwa kufanya ile inayo itwa" upinduaji" wa upasuaji. Katika miezi sita mengine, watu wengine sita walikutana naye, vile vile wakitaka pia kupinduliwa kwa upasuaji wao. (National Post).

Kama Waislamu tunaamini kuwa akili ya mwanadamu ina kikomo katika utambuzi juu ya maisha. Pia tunafahamu kwamba akili ya mwanadamu huathiriwa na mazingira iliyomo ndani yake na hivyo basi haina dawamu katika kufanya maamuzi. Ni kutokana na sababu hizi ambapo Waislamu hawaichukui akili ya mwanadamu katika kufikia uhakika thabiti wa ni nini sahihi na nini kosa au ni nini kheri na nini shari kwani yote haya daima hubalika na huwa na uwezo wa kupatikana dosari ya ni kitu gani kitakachomletea mtu binafsi na jamii kheri na furaha.

Fikra hii moja kwa moja hutokamana na Aqeedah yetu (ya kimaisha) inayo tufunza kwamba twahitaji kuwa na imani ya kukatikiwa kwa Allah (swt) na yale aliyotuteremshia kupitia Qur'an na Mtume wake Muhammad (saw) na kwamba kupitia yeye pekee ndio hujifunza kile kinachotakiwa kukadiriwa na kuonekana kuwa sahihi au kosa. Pia tunajifunza kuwa furaha imefungamanishwa moja kwa moja na kufuata muongozo kuhusiana na lile ambalo ni sahihi na kosa kwani hili ndilo litakalo pelekea utafutaji radhi za Allah na kupelekea Waislamu kupata furaha.

Kwa kufungamanisha ufahamu huu na yale tuliyopata katika makala ya juu, inadhihirisha wazi kuwa kumekuwa na ongezeko la wagonjwa wanaohisi majuto baada ya kufanyiwa upasuaji na urekebishaji wa nyeti zao, matokeo ya hili ni jambo ambalo kihakika lapaswa kuwa mshangao kwa Waislamu. Ama kwa mtazamo wa Kiislamu aina hizi za upasuaji ni haramu/makosa na kamwe hazipelekei kwenye mafaniko wala furaha katika maisha haya wala ya akhera, kutokana na yafuatayo: Imethibitishwa katika al-Sahih kuwa 'Abdallah ibn 'Abbas (ra) amesema:

**«لعن رسول الله صلى الله عليه وسلم المتشبهين من الرجال بالنساء، والمتشبهات من النساء بالرجال»**

**Mtume wa Allah (saw) amewalaani wanaume wenye kujifananisha na wanawake na wanawake wenye kujifananisha na wanaume.** (al-Bukhari).

Habari za watu kujutia kubadilisha jinsia zao kihakika zimekuja kama mshtuko kwa Profesa Djordjevic aliyehojiwa katika makala hayo na kama mtaalamu wa upasuaji na urekebishaji wa viungo vya uzazi aliposema: "Iinaweza kuwa janga la kikweli kusikia hadithi hizi". "Wale wanaotaka kupindua upasuaji huu, wameongea naye juu ya viwango vikubwa vya msongo wa mawazo kufuatia kipindi chao cha mpito baada ya upasuaji huo na katika kesi nyengine hata kufikiria kujiua." Daktari huyu ana hofu kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha maombi ya kutaka upinduaji wa upasuaji na pia ukosefu wa utafiti wa kielimu juu ya suala hili. Ameonyesha wasiwasi wake juu ya utaratibu unaofuatwa wakati wa kutoa maamuzi juu ya upasuaji huu.

Haya ndio haswa tunayo tarajia kwa mtu anaye liangalia suala hili kwa msingi wa aqeedah tofauti ya kimaisha isiyokuwa Aqeedah ya Kiislamu. Mfumo huru wa kimaisha wa kiilmani, aqeeda iliyojengwa juu ya msingi wa maridhiano na kutenganisha dini na maisha. Aqeeda inayoamua nini ni sahihi na nini ni kosa, kwa kutegemeza kipimo cha maslahi, inayopelekea kupatikana kwa kitendo, ambayo hutegemea furaha juu ya starehe za mwili anazopata mtu. Sasa basi ikiwa maslahi na furaha iliyopatikana kutokana na upasuaji wa aina hii yako chini ya uangalizi, fikra yote kuhusu utaratibu huu inahitaji pia kutathminiwa upya. Hili bila shaka ni jambo ambalo vuguvugu la kutetea ubadilishaji jinsia halingependa kulisikia kwani tunaposoma zaidi katika makala hayo yanaashiria kuwa ndilo sababu kubwa inayozuia vyuo vikuu kutofanya utafiti juu ya kadhia hii. Hii ni kwa sababu utafiti huu unavunjilia mbali porojo yao kuwa upasuaji huu ni jambo la lazima ili watu hawa waweze kupata furaha.

Ni muhimu kwa Waislamu leo, hususan wale wanaoishi nchi za magharibi kulielewa suala hili vyema kwani huenda wakakabiliwa na shinikizo kubwa la kukubali fahamu kama kadhia za ubadilishaji jinsia, ukhanithi, mahusiano ya kijinsia nje ya ndoa na kadhalika kama tabia zinazo kubalika ndani ya jamii.

Kivitendo hii humaanisha kwamba fikra hizi zitatekelezwa na kupigiwa debe ndani ya jamii kama haki ya mtu binafsi kutafuta na kutimiza starehe na furaha zao. Wataziwasilisha kwa kuruhusu haki hizi, kama ishara ya mtu au jamii ya kisasa, iliyoendelea, iliyo staarabika, na iliyo na uadilifu, na kwenda kinyume na haya kuoneka kama dhulma na ushamba kwa mtu binafsi au jamii.

Pindi sisi kama Waislamu, tutakapo fahamu maumbile yenye kikomo ya akili ya mwanadamu, na hatari za kuiruhusu kuamuru lipi ni sahihi na lipi ni kosa, na kwamba Allah pekee ndiye mwenye ujuzi kamili wa lipi ni zuri kwa watu binafsi pamoja na jamii – ndipo tutakapo weza kukataa shinikizo hizi za kukubali fahamu ambazo zinagongana na Uislamu wazi wazi.

**"Na hukumu baina yao kwa yale yote aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao. Nawe tahadhari nao wasije kukufitini ukaacha baadhi ya aliyo kuteremshia Mwenyezi Mungu. Na ikiwa wakigeuka, basi jua kwamba hakika Mwenyezi Mungu anataka**

*Endelea Uk..10*

kuwasibu kwa baadhi ya dhambi zao. Na hakika wengi wa watu ni wapotofu.” [Al-Maaida: 49]

**Yasmin Malik**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**



# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

# Halaqa 6: Propaganda ‘Uvumi’ Dhidi ya Mtume (saw) na Da’wah yake

Katika halaqa hii tutazungumzia mbinu ya pili ambayo wameitumia Maqureysh dhidi ya da’wah ya Mtume (s.a.w) nayo ni Propaganda ‘Uvumi’ dhidi ya Mtume (s.a.w) na da’wah ya Qur’an.

Walipoona Maqureysh kuwa Mtume (saw) hakuna kinachomzuia na da’wah yake walianza kumchezashere kumfanyia mizaha na kumkadhibisha,na hayo ni kwa madai yao kuwa ati ni mchawi, kuhani, mshairi, na kumzushia mengine mengi. Qur’an ilisajili propaganda/ uvumi huo; kama ifuatavyo: Asema Allah (swt):

بَلْ قَالُوا أَضْغَاثُ أَحْلَامٍ بَلِ افْتَرَاهُ بَلْ هُوَ شَاعِرٌ فَلْيَأْتِنَا بِآيَةٍ كَمَا أُرْسِلَ الْأَوَّلُونَ

Lakini wao walisema: Hizo ni ndoto za ovyo ovyo, bali amezizua tu, bali huyo ni mtunga mashairi. Basi atuletee miujiza kama walivyo tumwa wale wa mwanzo [Al-Anbya 21:5]

أَمْ يَقُولُونَ شَاعِرٌ نَتَرَبَّصُ بِهِ رَيْبَ الْمَنُونِ

Au wanasema: Huyu ni mtunga mashairi, tunamtarajia kupatilizwa na dahari.
[At-Tur: 30]

وَقَالُوا يَا أَيُّهَا الَّذِي نُزِّلَ عَلَيْهِ الذِّكْرُ إِنَّكَ لَمَجْنُونٌ

Na walisema: Ewe uliyeteremshiwa Ukumbusho! Hakika wewe ni mwendawazimu
[Al-Hijr: 6]

Baada ya kusajiliwa propaganda ‘uvumi’ zao kisha zilijibiwa na Qur’an kama ifuatavyo; Asema Allah (swt)

فَلَا أُقْسِمُ بِمَا تُبْصِرُونَ

Basi naapa kwa mnavyo viona,

وَمَا لَا تُبْصِرُونَ

Na msivyo viona,

إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ

Kwa hakika hii ni kauli iliyoletwa na Mjumbe mwenye hishima.

وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَاعِرٍ ۚ قَلِيلًا مَا تُؤْمِنُونَ

Wala si kauli ya mtunga mashairi. Ni machache sana mnayo yaamini.

وَلَا بِقَوْلِ كَاهِنٍ ۚ قَلِيلًا مَا تَذَكَّرُونَ

Wala si kauli ya kuhani. Ni machache mnayo yakumbuka.

تَنْزِيلٌ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ

Ni uteremsho utokao kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.

وَلَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا بَعْضَ الْأَقَاوِيلِ

Na lau kama angelituzulia na baadhi ya maneno tu,

لَأَخَذْنَا مِنْهُ بِالْيَمِينِ

Bila ya shaka tungelimshika kwa mkono wa kulia,

ثُمَّ لَقَطَعْنَا مِنْهُ الْوَتِينَ

Kisha kwa hakika tungeli mkata mshipa mkubwa wa moyo!

فَمَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ عَنْهُ حَاجِزِينَ

Na hapana yeyote katika nyinyi ambaye angeliweza kutuzuia.

وَإِنَّهُ لَتَذْكِرَةٌ لِلْمُتَّقِينَ

Kwa hakika huu ni ukumbusho kwa wachamungu.

*Endelea Uk..11*

وَإِنَّا لَنَعْلَمُ أَنَّ مِنْكُمْ مُكَذِّبِينَ
Na hakika Sisi bila ya shaka tunajua kwamba miongoni mwenu wapo wanao kadhibisha.

وَإِنَّهُ لَحَسْرَةٌ عَلَى الْكَافِرِينَ
Na hakika bila ya shaka itakuwa ni majuto kwa wanao kataa.

وَإِنَّهُ لَحَقُّ الْيَقِينِ
Na hakika hii bila ya shaka ni haki ya yakini.

فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ
Basi litakase jina la mola wako Mlezi Mtukufu.
[Al-Haaqqa: 38-52]

Qur'an imeelezea kwa picha ya wazi kabisa kuhusu msimamo wa Waleed bin Mughira. Akijaribu kufikia maneno ya upambanuzi ambayo yanaonyesha msimamo wa wenye inadi kama yeye ambao walikuja kwake wakimtaka awape kauli kuhusu Qur'an kauli ambayo wataafikiana kwayo Maqureysh kuwakabili wageni wanaokuja hija watakapowauliza khabari za Mtume (s.a.w) na Qur'an ambayo inamteremkia:

Akasema Ta'ala:

كَلَّا ۖ إِنَّهُ كَانَ لِآيَاتِنَا عَنِيدًا
Hasha! Kwani hakika yeye alikuwa akizifanyia inadi Aya zetu!

سَأُرْهِقُهُ صَعُودًا
Nitamtesa kwa mateso yasio wezekana.

إِنَّهُ فَكَّرَ وَقَدَّرَ
Kwani hakika yeye alifikiri na akapima.

فَقُتِلَ كَيْفَ قَدَّرَ
Basi ameangamia! Vipi alivyo pima!

ثُمَّ قُتِلَ كَيْفَ قَدَّرَ
Tena ameangamia! Vipi alivyo pima!

ثُمَّ نَظَرَ
Kisha akatazama,

ثُمَّ عَبَسَ وَبَسَرَ
Kisha akakunja kipaji, na akanuna.

ثُمَّ أَدْبَرَ وَاسْتَكْبَرَ
Kisha akaipa kisogo haki, na akatakabari.

فَقَالَ إِنْ هَٰذَا إِلَّا سِحْرٌ يُؤْثَرُ
Na akasema: Haya si chochote ila ni uchawi ulio nukuliwa.

إِنْ هَٰذَا إِلَّا قَوْلُ الْبَشَرِ
Haya si chochote ila kauli ya binaadamu.

سَأُصْلِيهِ سَقَرَ
Nitakuja mtia kwenye Moto wa Saqar.

وَمَا أَدْرَاكَ مَا سَقَرُ
Na nini kitakujulisha ni nini huo Moto wa Saqar

لَا تُبْقِي وَلَا تَذَرُ
Haubakishi wala hausazi

لَوَّاحَةٌ لِلْبَشَرِ
Unababua ngozi iwe nyeusi.

[Al-Muddaththir: 16 – 29]

Na mwisho baada ya taabu zote hizi, na bidii zote, na mashaka asema Waleed bin Mughira maneno yake ya mwisho kuhusu Qur'an. Na lau maneno haya yatatambulisha chochote basi yatakuwa yanatambulisha muujiza wa Qur'an na daraja yake ya juu. Akasema waleed:

"Wallahi nimesikia maneno kwa Muhammad si maneno ya mwanadamu, wala maneno ya jini, Wallahi maneno yake yana utamu, na yana mvuto, ni sawa na mti wenye matunda mingi juu yake na mizizi chini imekita. Na hakika yako juu wala hakuna kinachokuwa juu zaidi yake".

Itaendelea katika UQAB Toleo 11…In Shaa Allah.

# SWALI / JAWABU: Kilicho Nyuma ya Kura ya Maoni Juu ya Kulitenga Eneo la Kurdistan

**Swali:**
Ni kwa nini Barzani anasisitiza kufanyika kwa kura ya maoni ya kuutenga mkoa wa Kurdistan, licha ya kuwa hakuna uidhinishwaji wa kimataifa au wa kieneo wa kura hii ya maoni? Kulingana na dhurufu zilizoko kwa sasa si kura hii ya maoni iko dhidi ya matakwa ya Wakurdi wenyewe? Je kura hii ya maoni inatarajiwa kufanyika? Ikiwa kura hii ya maoni itafanyika na wengi wakaipitisha, inawezekana kubuniwa kwa serikali ya Kikurdi katika eneo hili? Jazakum Allah Khairan.

**Jibu:**

**Kuna msemo usemao ikiwa mtawala atachukua uamuzi kinyume na maslahi ya nchi yake, humaanisha kuwa mtawala huyo ni kibaraka, na kwamba uamuzi huo huwa umeshurutishwa na dola nyengine kwa ajili ya maslahi yake… maneno haya yanashabihiana kwa karibu na hali ya Wakurdi katika eneo la Kurdistan, ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo:**

1 - Mwanasiasa yeyote aliye makinika anaelewa ni vigumu kiasi gani kwa Wakurdi kuwa na dola yao. Ukweli ni kuwa, kampeni ya kubuni dola ya Wakurdi katika dhurufu za kimataifa zilizoko kwa sasa ni haribifu kwa mkoa wa Kurdistan, sio tu kisiasa na kimaadili, bali pia uharibifu wa kimada. Kwani kadhia iliyoko sio juu ya kubuniwa kwa dola ya Wakurdi nchini Iraq, na kama hiyo ndiyo ingekuwa kadhia, basi ingewezekana…

Serikali iliyoundwa na Waamerika baada ya uvamizi wa Iraq, iliyokuja kutambulika kama katiba ya Bremer, serikali hii imeifanya Iraq kuwa mkusanyiko wa majimbo ya mkoa yaliyo na mahusiano tete na serikali kuu, mpaka ikaifanya idara ya jimbo la Kurdistan kuwa na nguvu zaidi kushinda serikali kuu jijini Baghdad katika upande wa utawala na usimamizi wa eneo hilo! Dhamira ya dola za kikafiri za kikoloni akilini mwao ni kupanda mbegu za kugawanya na kuvunja vunja biladi yoyote ya Waislamu wanayo ivamia, lakini husubiri tu kutokea kwa fursa muwafaka, yote haya yakitokana na chuki yao dhidi ya Uislamu na Waislamu… tumeeleza katika jibu la swali lilio tangulia la tarehe 12/8/2017:

"*-Amerika tangu uvamizi wake wa Iraq mnamo 2003 inaendelea kufanya kazi kuivunja vunja Iraq; katiba ambayo Bremer ameiweka kwa msingi wa ki-madhehebu imeweka eneo kwa kila dhehebu… Aligawanya kwa ushirikiano, na raisi, na kiongozi wa bunge, na waziri mkuu, na kwa kuwa waziri mkuu ndiye aliye na mamlaka ya utekelezaji, na kwa kuwa Bremer ameiunda kwa msimamo wa ki-madhehebu iligeuka kuwa nukta ya utesi na uchochezi kwa wadau wengine… kielelezo cha katiba yenyewe kinaieleza serikali kuwa ya majimbo juu ya maeneo, na kwamba mamlaka ya majimbo hayo ndiyo yenye nguvu. Kwa hivyo, Amerika imefaulu kuunda dhurufu za kuivunja vunja Iraq kimaeneo…*" Mwisho.

Mkoa huu kivitendo ni dola lakini isiyokuwa na afisi za ubalozi wala uanachama katika Umoja wa Mataifa na taasisi nyengine mfano wake… Ama kwa hali halisi, eneo la Kurdistan ni dola ndani ya dola iliyotenganishwa barabara na serikali kuu, kutokana na kuwekwa mbali Iraq kuwa kama dola moja! Hivyo basi, eneo la Kurdistan halihitaji dola ndani ya Iraq kwa kuwa kivitendo tayari ni dola… Na kama tulivyosema, kadhia sio kubuniwa kwa dola ya Kikurdi ndani ya mipaka ya eneo la Kikurdi nchini Iraq na wala haihusiani lolote na maeneo mengine ya Kikurdi nje ya Iraq, hii sio kadhia. Badala yake, ikiwa itaundwa dola yoyote ya Wakurdi, bila shaka nyuma yake itavutia harakati nzito za Wakurdi kati eneo hilo, ili dola hiyo ya Kikurdi isisimame katika eneo la Kurdistan… Hivyo basi, hili likitokea litakuwa ni pigo uchungu, hususan kwa Amerika na vibaraka wake nchini Uturuki, Iran na Syria. Kwa hivyo, mwanasiasa yeyote anajua kwamba kuundwa kwa dola ya Wakurdi, ima nchini Uturuki, Iraq au Syria, kwa sasa hakutavumiliwa kutokana na masharti ya kimataifa au ya kieneo, na kamwe hakumaanishi kuwa wanasiasa wa Kikurdi, wakiwemo Al-Barzani, hawatambui hili. Bali, kama ilivyo tangulia kutajwa, wazo la kuunda dola ya Kikurdi katika dhurufu zilizoko sasa huenda ikapelekea kutokea kwa mabadiliko ya mipango na harakati zisizo dhibitika katika eneo hilo, hususan eneo la Wakurdi. Ambalo, kama tulivyo sema, itawaathiri sio tu kimaadili na kisiasa bali pia kimada, na hivyo basi uamuzi wa Barzani uko dhidi ya maslahi ya nchi yake katika dhurufu zilizoko kwa sasa… **Hii ndio sehemu ya kwanza ya maneno.**

2- Kuhusiana na ni dola ipi iliyoko nyuma ya uamuzi wa Barzani, kwamba uamuzi huu ni kwa ajili ya maslahi ya dola hiyo, dalili ziko wazi katika hili, na si vigumu kulekeza kidole kutambua ni dola ipi hii. Tangazo la kura ya maamuzi kuunda dola kando kutoka Iraq, haliwezi kutolewa na Barzani huku kukiwa na upinzani dhidi ya Amerika na upinzani kutoka kwa dola za eneo zinazolizunguka eneo la Kurdistan ambalo ni tiifu kwa Amerika. Hawezi kupata nguvu ya kukabiliana na nguvu hizi pinzani, isipokuwa kuwe na dola nyengine kuu inayomsaidia Barzani na kumshajiisha kuchukua uamuzi huu. Kwani eneo lote la Kurdistan, ni dhaifu sana kusimama dhidi ya dola hizo, hususana Amerika, inayo idhibiti Iraq yote. Si vigumu, kama tulivyo tangulia kusema mwanzoni, kutambua kwamba dola hii kubwa inayo simama nyuma yake na kumpa maagizo kufanya maamuzi hayo ni Uingereza. Familia ya Barzani imenasibishwa na Uingereza tangu dola ya Kiuthmani. Barzani alirithi mahusiano haya kutoka kwa babake, Mustafa Mulla Barzani, na kabla yake ami yake Ahmed Barzani na

*Endelea Uk..13*

kabla yao Abdul Salam Barzani, iliye ongoza uasi wa kisilaha dhidi ya dola ya Kiuthmani kuanzia mnamo 1909 mpaka 1914 akiwa na usaidizi wazi kutoka kwa Uingereza. Kwa hivyo, familia hii ina mahusiano ya muda mrefu na Uingereza… ikiwa tutafuata misimamo katika kura hii ya maamuzi, tutaona kuwa msimamo wa Uingereza ulikuwa ukipendelea uamuzi wa kura ya maamuzi, ingawa Uingereza inatambulika kwa mbinu yake ovu na uhadaifu:

**Kwa mfano,** Barzani alikutana na Frank Baker, Balozi wa Uingereza nchini Iraq mnamo 24/8/2017 kuelezea usaidizi wa Uingereza kwake. Tovuti ya kikurdi "Rudaw" iliripoti mnamo 24/8/2017, habari za mikutano hii, "Wakati wa mkutano wa Barzani na balozi wa Uingereza nchini Iraq, mgeni huyu (balozi) alielezea kuelewa kwa nchi yake juu ya haki za watu wa eneo la Kurdistan, na kumdokezea raisi wa eneo la Kurdistan kuhusu msimamo wa Uingereza wa kufanywa kwa kura ya maamuzi." Maana ya kuelewa kwa lugha ya kidiplomasia ni kusaidia, na maana ya kumuelezea kuhusu msimamo wa Uingereza pasi na kutaja chochote pia ni kusaidia. Yaani, msimamo wa Uingereza una unga mkono uamuzi wa Barzani, bali unatoa usaidizi kwake na kumwambia aendelee nao licha ya upinzani wa Amerika na nchi zinazo egemea upande wa Amerika katika eneo hilo.
**Mfano mwengine,** afisa wa mahusiano ya kigeni katika eneo la Kurdistan Falah Mustafa alisema katika shirika la habari la Kurdistan 24 kuwa "Uingereza haiko dhidi ya kura ya maamuzi, na wala haipingi matarajio ya Wakurdi." Hotuba ya Mustafa ilikuja baada ya mkutano wa Waziri wa Kigeni wa eneo la Mashariki ya Kati na Kaskazini mwa Afrika, Alistair Burt pamoja na maafisa wa Kikurdi mjini Erbil. Waziri huyu wa Kigeni wa Uingereza wa eneo la Mashariki ya Kati na Kaskazini mwa Afrika aliwasili mjini Erbil mnamo Jumapili kwa mazungumzo na maafisa wa Kikurdi juu ya kadhia kadha wa kadha. Mpango wa Wakurdi kufanya kura ya maamuzi juu ya kulitenga eneo la Kurdistan kutoka kwa Iraq mnamo 25 Septemba ni hatua ya kwanza ya kubuni serikali huru. (Kurdistan 24 Arbil, 5/9/2017).

**Hivyo basi, Uingereza ndio nchi iliyo nyuma ya uamuzi wa kura ya maamuzi uliotolewa na Barzani.**

3 – Ama kuhusu maslahi ya Uingereza katika uamuzi huu, ni yenye kuendelea tangu Trump kushinda katika uchaguzi na Waziri Mkuu wa Uingereza May kuharakisha kumzuru Trump mnamo 26/1/2017 na kumpomgeza jijini Washington… Wakati huo, Trump alimsifu May na vile vile May alimsifu Trump, lakini kila mmoja alikuwa na lengo tofauti na mwengine! Ama Trump, alitaka Uingereza kufanya bidii iwezavyo kuuvunja Muungano wa Ulaya, ili iweze kuvunja mahusiano yake na Ulaya kimasomaso. Wakati huo huo, kutoa juhudi kuunda mazingira muwafaka ya kuvunja Muungano wa Ulaya, hususan nchi ya Ufaransa na Uholanzi, ambazo zilikuwa ukingoni mwa kura hizo. Ama May, alitaka makubaliano ya kibiashara kutoka kwa Trump kupatiliza katika shinikizo mpya juu ya nchi za Muungano wa Ulaya ili ijishindie biashara wakati itakapo jiondoa katika Muungano huo. Wakati wa ziara hii, Trump na May waliangazia dhamira ya malengo yao. May, kama ilivyo ada ya Uingereza, alijaribu kuficha lengo lake la kibiashara kwa njia za kinafiki, lakini kwa ukosefu wa diplomasia wa Trump na matamshi yake ya wazi hayaku muwezesha May kuficha nia zake…

Hivyo basi, pindi nchi zinazounga mkono Muungano wa Ulaya ziliposhinda kura chini ya Uholanzi na Ufaransa, na kwa kuongezea kuwa Ujerumani inaunga mkono kwa dhati Muungano wa Ulaya na kuupatia umakinifu wa hali ya juu, ilimfanya Trump kutambua kuwa hamu ya Uingereza ilikuwa tu kukamilisha makubaliano ya kibishara na Amerika na wala haikulitia maanani suala la kuvunja Muungano wa Ulaya kama alivyo taka Trump na yote haya yalipelekea majibu makali kutoka kwa Trump, natija yake ikiwa ni kuchapwa kwa Uingereza nchini "Qatar" kupitia kuzingirwa kivikwazo na kutengwa! Tayari tumeshafafanua hili katika jibu la swali tulilotoa mnamo 23/7/2017, ambapo tulisema:
"*Kuhusiana na Uingereza: ziara ya mwanzoni ya Waziri Mkuu wa Uingereza Theresa May jijini Washington mnamo Januari 26, 2017 na hamu yake ya kutaka kutia saini makubaliano ya kibiashara na Washington itakuwa kama kielelezo kwa nchi nyenginezo za Muungano wa Ulaya kuzishajiisha kuondoka katika Muungano wa Ulaya. Hivyo basi, Uingereza ilidumisha kushikana kwake na Amerika na iliipendelea zaidi idara ya Trump, lakini baada ya matarajio ya Amerika ya kuuvunja Muungano wa Ulaya kuchanika, kama ilivyo shuhudiwa katika ushindi wa upande unaounga mkono Muungano wa Ulaya katika kura nchini Uholanzi na Ufaransa, mtazamo mzuri wa Trump kwa Uingereza ulibadilika kwa kuwa aliitaka iongoze mchakato wa kuivunja Ulaya, na pindi hali ya kujiondoa kwa Uingereza ilipokosa kujirudia jijini Paris na Amsterdam, Amerika imerudi tena kuchafua maslahi ya kimataifa ya Uingereza katika namna iliyoishtua London. Amerika inamsukuma kibaraka wake, Sisi, kuongeza usaidizi wake kwa Hafter bila ya kuzingatia maslahi ya Uingereza nchini Libya, na Amerika ikawasukuma vibaraka wake katika njia ya mshtuko kiasi kuishinikiza Qatar, ambayo ni kibaraka wa Uingereza eneo la waarabu na Uislamu...*" Mwisho

Yote haya yalimfanya Trump kuhamaki na kufanya ziara ya haraka nchini Saudi Arabia na kufanya kongamano lile na kisha kuigonga Uingereza kupitia kuizingira kivikwazo na kuikata Qatar.

4 – Hapa, ilikuwa ni muhimu kwa Uingereza kukatiza baadhi ya maslahi ya Amerika katika eneo hili, kwa hivyo iliamua kutumia uamuzi wa Barzani kuitisha kura ya maamuzi kuiudhi Amerika na vibaraka wake.

*Endelea Uk..14*

Na bila shaka, Uingereza inaweza tu kuikatizia Amerika, kwani haina uwezo wa kukabiliana na Amerika paruwanja, lakini inaweza kuikatizia na kuiudhi, hususan ikiwa itachagua hali muwafaka na kazi barabara kama ilivyo pata ndani ya kura ya maamuzi ya Kurdistan. Uingereza ilikuwa makini kwa Barzani kufuata njia iliyo muekea kwa sababu hali iliyoko kwa sasa ni moto kwa Amerika pamoja na vibaraka wake; Uturuki, Iran na Syria kwa sababu ya harakati za kisilaha zinazoendelea… kwa hivyo Barzani alidumu kusisitiza juu ya kura ya maamuzi na Uingereza ikaifanyia propaganda kura hii ya maamuzi kuwa ndiyo itakayo faulu kupatikana kwa dola huru ya Wakurdi katika eneo la Kurdistan. Na kama ilivyo kawaida ya ujanja na unafiki wake, Uingereza haitilii maanani kupatikana au kutopatikana maslahi ya Wakurdi maadamu tu itafaulu kufikia maslahi yake binafsi, na historia ya Uingereza na Wakurdi imesheheni mambo haya!

**Tulisema katika jibu la swali la tarehe 1/4/2009:**
"… *Uingereza ilimuahidi Mahmood Al-Hafeed dola ya Kikurdi mnamo 1919 Miladi baada ya kupigana na majeshi ya dola ya Kiuthmani eneo la Sulaimaiyyah. Majeshi ya Al-Hafeed yakapigana, yakawaua ndugu zao wa Kiuthmani na kuwafurusha, lakini bila shaka Uingereza haiku khini tu ahadi yake, bali pia ilimfukuza Al-Hafeed na kumpeleka katika koloni yake ya India. Vile vile katika mkataba wa Sèvres mnamo 1920, Uingereza iliisisitiza dola ya Kiuthmani kujumuisha kifungu kinachohusu dola ya Kurdistan kwa lengo la kumtia dhiki Khalifa Muhammad Waheeduddin. Katika mkataba huu, ujumbe wa Khalifa ndio uliokuwa ukijadiliana. Uingereza ilipo faulu kuivunja Khilafah na kumuweka kibaraka wake Mustafa Kamal kama raisi wa Jamhuri ya Uturuki, na baada ya kutia saini mkataba wa Lausanne pamoja nayo mnamo 1924, Uingereza ilikataa kujumuisha kifungu cha dola ya Kikurdi na sababu yake nyepesi ikiwa: tayari ishafaulu kufikia lengo lake, ambalo bila shaka ni kuivunja dola ya Khilafah, kwa hivyo ahadi hii sasa imepitwa na wakati! Uingereza ndiyo iliyo chochea hamasa na miito ya kikabila ya Kikurdi pamoja na 'matarajio' yote mengine ya kikabila katika eneo zima (la ulimwengu wa Kiislamu), na ni Uingereza vile vile iliyo patiliza hamasa hizi na kuwashinikiza kupigana na kuasi dhidi ya dola ya Kiislamu ili Uingereza iweze kufikia malengo yake. Hatimaye ikazitumia hamasa zote hizi kwa kushirikiana nao na kuwatumia kama vibaraka wake na kuwaweka mamlakani kama watawala na viongozi katika biladi hizo…*" **Mwisho**. Huu ndio ujanja na khiyana ya Uingereza…

5- Hivyo basi, Barzani amesisitiza kufanyika kwa kura ya maamuzi mnamo 25/9/2017, ili awe na dola! Kamwe hakutilia maanani upinzani wa kimataifa au wa kieneo uliopinga kura hiyo, hata kutoka kwa miongoni mwa Wakurdi wenyewe, badala yake akasema: (Eneo la Kurdistan limekariri tena mnamo Jumatano kupinga kwake kuakhirishwa au kufutiliwa mbali kwa kura hii ya maamuzi ya uhuru kutokana na Iraq iliyo pangwa kufanyika mnamo Septemba 25, licha ya juhudi za kimataifa na kieneo za kuisihi Erbil kuachana na hatua hii, na kukataa kwa serikali kuu jijini Baghdad kura hii na matokeo yake.

Baraza Kuu la kura hii ya maamuzi katika eneo la Kurdistan, wakati wa mkutano ulioongozwa na raisi Masoud Barzani, jana, lilijadili matokeo ya ziara ya ujumbe wa Kurdistan jijini Baghdad, kuhusiana na suala la kura ya maamuzi, pamoja na matokeo ya mazungumzo kati ya Barzani na Mattis mjini Erbil, juzi. Mshauri wa Barzani alisema: raisi Masoud Barzani amesema kuwa kura ya maamuzi kamwe haita akhirishwa na itafanyika mnamo Alhamisi 25 Septemba sawia na 2 Dhu al-Hijja 1438 Hijri – 24 Agosti 2017 Miladi – Dubai – al-arabiya.net). Hii ni pamoja na ufahamu wa upinzani wa kimataifa na kieneo kuwa wazi kabisa:

A – Amerika ilipinga kura hii ya maamuzi kuanzia siku ya kwanza Barzani alipotangaza kufanyika kwake, ambapo mnamo 7/6/2017 alitangaza kuwa kura ya maamuzi ya kuasisi dola huru ya Kikurdi itafanyika katika maeneo ya Wakurdi nchini Iraq mnamo 25 Septemba. Amerika ilijibu kupitia mjumbe wa raisi wa Amerika katika muungano wa kimataifa, Bert Mc Gurk: "Hatuoni haja ya kufanyika kwa kura ya maamuzi mnamo Septemba kwa sababu itazua hali ya wasiwasi. Kufanywa kura ya maamuzi kwa njia hiyo ya haraka, haswa katika maeneo yenye mizozano, kwa madhanio yetu, itazua wazi hali ya wasiwasi." (AFP, 8/6/2017)
Hivi majuzi, Waziri wa Kigeni wa Amerika Rex Tillerson mnamo 11/8/2017 katika maongezi ya simu na raisi wa eneo la Kurdistan Masoud Barzani, alieleza "hamu ya Washington kuakhirisha kura ya maamuzi ya uhuru wa eneo hilo na kuunga kwake mkono kuendelea kwa mazungumzo na majadiliano baina ya eneo hilo na Baghdad." Amerika ilituma waziri wake wa ulinzi James Mattis jijini Baghdad mnamo 22/8/2017 kukutana na Waziri Mkuu wa Iraq Abbadi na kisha kwenda Erbil na Ankara mnamo 23/8/2017 kuisukuma Uturuki, mkono wake imara katika eneo…

B – Serikali za eneo zilizotiifu kwa Amerika pia zimepinga… Msemaji wa Waziri Mkuu Saad al-Hadithi alisema "Uamuzi wowote unaohusu mustakbali wa Iraq ni lazima uzingatie vipengee vya katiba kwa kuwa ni uamuzi wa Iraq, kikatiba Iraq imefafanuliwa kama taifa la kidemokrasia, la kimajimbo na lenye ubwana kamili… Wairaqi wote ni lazima wawe na kauli juu ya mustakbali wa nchi yao. Hakuna yeyote atakaye waamulia hatma yake bila ya wao kuhusishwa." (Free American 9//6/2017).
Uturuki imetangaza upinzani wake kwa kura hii ya maamuzi ya kutangaza uhuru wa Kurdistan kuanzia siku ya kwanza, kwa hayo Waziri wa Kigeni wa Uturuki akatoa taarifa kuelezea uamuzi wa raisi wa mkoa (wa Kurdistan) kama "kosa

***Endelea Uk..15***

baya mno na wenye kuhatarisha umoja na hadhi ya eneo la Iraq" (Free American 9/6/2017) ... Erdogan alitangaza baada ya mkutano na Waziri wa Ulinzi wa Amerika Mattis na kusema: "Uamuzi huu wa kura ya maamuzi ni wa kimakosa" (Al-Jazeera 24/8/2017)… Vile vile Iran ikatangaza, mnamo Jumamosi, 11 Juni 2017, muda mfupi baada ya tangazo la kura ya maamuzi, kuwa inapinga vikali kufanyika kwa kura hii ya maamuzi katika maeneo ya Wakurdi nchini Iraq Septemba ijayo. Ikisisitiza kuwa Tehran ina msimamo wazi juu ya umoja wa maeneo ya Iraq. Msemaji wa Waziri wa Kigeni wa Iran, Bahram Qasimi, alisema: "Maamuzi mapana ya upande mmoja ambayo ni sehemu ya vipimo halali vya kitaifa, yatapelekea matatizo zaidi na kudorora zaidi kwa hali ya usalama nchini Iraq." (15/6/2017 http://afkarhura.com). Tovuti ya fikra huru ya http://afkarhura.com/?p=6839 ilichapisha mnamo 7 Septemba 2017, taarifa ya raisi wa baraza la shura la Iran, ambayo ilisema: "Raisi wa Baraza la Kiislamu la Shura katika masuala ya kimataifa, Hussein Amir Abdullahian, amethibitisha kuwa kura ya maoni katika eneo la Kurdistan nchini Iraq itasababisha kuzuka kwa mgogoro mpya."

Zaidi ya hayo, Amerika ina wafuasi ndani ya Kurdistan, ikiwemo harakati ya Kikurdi ya Goran (chama cha mabadiliko) na chama cha umoja wa kitaifa cha Talabani. Harakati ya Goran imepinga tangazo la Barzani la kura ya maamuzi, haya yamesemwa na Hoshyar Abdullah mwanachama wa harakati hiyo katika bunge la Kurdistan: "Harakati ya mabadiliko bado inashikilia rai ile ile kwamba huu sio wakati muwafaka kwa kura ya maamuzi na ajenda hii ni ya kibinafsi na ya chama cha Masoud Barzani" akisisitiza kuwa "Chama cha Kidemokrasia cha Kurdistan (KDP) ni kibaraka na wala si mshika dau." (Elaph, 5/8/2017)

Vile vile, raisi wa Jamhuri ya Iraq Fuad Masum, anayetoka katika Chama cha Kitaifa cha Kidemokrasia cha Talabani alipinga kura hii ya maamuzi, akisema: "Afisi ya raisi imekuja kuwasaidia Wakurdi, kura za Wakurdi kamwe hazilingani na tone la damu yao na kujitolea muhanga kwao na hivyo haitaruhusu ndoto ya "Masum" ya kuasisi dola yao na itakabiliana nayo siku ya kura ya maamuzi." Chama cha Kidemokrasia cha Kurdistan (KDP) kilisema katika taarifa kufafanua taarifa ya Masum kuwa "taarifa hatari na ujumbe mbaya kwa nchi za kiulimwengu zuieni matokeo ya kura hii ya maamuzi na muidunishe." (Kutoka katika chanzo kilichotangulia).

Licha ya upinzani huu wa kieneo na kimataifa, Barzani anasisitiza kufanyika kwa kura ya maamuzi na kutangaza kuwa hataichelewesha hata kwa dakika moja, kama tulivyo tangulia kutaja juu. Yote haya ni kwa sababu ya msukumo wa Uingereza katika suala hili la kura ya maamuzi kama tulivyo onyesha kwa kuirudia upya hali hii.

6 – **Sasa baada ya kurudia upya matukio ya kura hii ya maamuzi inayo athiriwa na mambo kadha wa kadha… Sasa twaweza kujibu matarajio ya kura hii… Linalo tarajiwa zaidi katika hili, na kutoka katika yale tuliyo yaangazia ni kama ifuatavyo:**

A. Katika hali zote, haitarajiwi kuwa dola ya Kikurdi itabuniwa kwa sura halali kama dola, kwa sababu mradi wa Kiamerika wa Iraq ni kuifanya Iraq kuwa serikali ya kimajimbo ya mikoa yenye mahusiano tata baina ya majimbo na serikali kuu. Hili lamaanisha, kivitendo kuna kutenganishwa kati ya utawala na usimamizi wa Iraq, huku rasmi ikibaki kuwa serikali ya kimajimbo ya mikoa kwa jina Iraq… Huu ndio mradi wa Kiamerika kwa Iraq tangu uvamizi wake mnamo 2003, ambao imekuwa ikibeba mbegu za kuigawanya na kuivunja vunja Iraq, pasi na kuzitangaza rasmi kuwa dola huru, bali itafanya hivyo wakati muwafaka utakapowadia. Bremer, gavana wa Amerika nchini Iraq, hatimaye akaweka katiba ya kimajimbo ya mikoa ya Iraq, ikaiangamiza hadhi ya Iraq kuwa kama dola moja yenye nguvu na mamlaka moja makuu, na kuibadilisha kuwa dola hafifu ya kimajimbo, ambayo mamlaka ya mikoa yana nguvu zaidi kuliko mamlaka katika serikali kuu! Ili Iraq itayarishwe, katika wakati ambao Amerika itauona kuwa muwafaka kwa maslahi yake binafsi, na ili itayarishwe kufanywa rasmi kuwa vijidola kadhaa kutokana nayo… Ama kwa sasa, mradi huu wa Kiamerika ni kubaki kuwa serikali ya kimajimbo ya mikoa ya Iraq katika hali ya mahusiano tata na serikali kuu… Tumetoa katika jibu la swali lililotangulia la tarehe 12/8/2017 linalosema:

"*-Amerika tangu uvamizi wake wa Iraq mnamo 2003 inaendelea kufanya kazi ya kusababisha kuvunjika vunjika kwake; katiba ambayo Bremer ameiweka katika msingi wa madhebevu imegawanya sehemu kimadhehebu… Amezigawanya baina ya Raisi, kiongozi wa bunge na Waziri Mkuu, na kwa sababu Waziri Mkuu ndiye mtu aliye na mamlaka ya utendaji, na kwa kuwa msimamo alio uweka Bremer ni wa kimadhehebu ili geuka kuwa chuki na uchochezi kwa wadau wengine… kielelezo cha katiba chenyewe chaeleza kuwa serikali ni ya majimbo juu ya maeneo, na nguvu za majimbo haya ziko imara. Hivyo basi, Amerika imefaulu kuunda dhurufu za kuivunja vunja Iraq kuwa majimbo matatu*…" **Mwisho**

Hivyo basi, sera ya sasa ya Kiamerika haitaki kuwepo kwa dola ndani ya Iraq, bali inachotaka ni kuwepo kwa serikali dhaifu ya majimbo, iliyogawanyika katika upande wa utendakazi huku kimuundo ikibakia kama dola moja. Kwa haya, haitarajiwi katika dhurufu zilizoko kwa sasa kuigawanya Iraq rasmi, bali Iraq inabaki kuwa kwa mujibu wa Bremer mradi ambao kivitendo imegawanyika na mikoa yake ina nguvu kuliko serikali kuu! Angalau kwa mustakbali wa karibu.

B – Kwa kuwa tangazo la kura ya maamuzi ni agizo la Uingereza kukwepa tatizo la Uingereza kutokana na yale yaliyotokea kwa Qatar, basi, kura hii ya maamuzi

*Endelea Uk..16*

itafutiliwa mbali ikiwa Amerika itasaidia katika kusitisha kutengwa kwa Qatar au hata kuipa afueni kwa njia muwafaka kuuokoa uso wake…

C – Amerika yaweza kufutilia mbali kura hii ya maamuzi ikitaka, kwa sababu ni nchi pekee inayo idhibiti Iraq. Ima ufutiliaji mbali huu wa kura ya maamuzi ufanywe moja kwa moja na Amerika, au kwa kuzisukuma harakati za Kikurdi zilizo tiifu kwake katika eneo la Kurdistan, au kwa kuisukuma Uturuki na Iran dhidi ya eneo hilo na, dhidi ya Barzani hata ikibidi utumiaji nguvu katika ushinikizaji. Mkuu wa jeshi la Iran, Mohammad Baqri, alizuru Uturuki kwa mara ya kwanza tangu kuasisiwa kwa Jamhuri ya Iran mnamo 1979. Ziara hii ilifanyika mnamo 15/8/2017, na ilichukua siku tatu. Alipokewa na Raisi wa Uturuki Erdogan katika makao ya Raisi jijini Ankara na mkutano ukachukua dakika 50, kama ilivyo ripotiwa na shirika rasmi la habari la Uturuki la Anatolia agency, ukionyesha umuhimu wa jambo hili. Mkuu wa jeshi la Iran aliandamana na mkuu wa kikosi cha wanajeshi wa nchi kavu na kamanda wa kikosi cha walinzi wa mipaka wakiwemo pia makamanda kadhaa wa kijeshi wa ngazi za juu wa Iran, shirika rasmi la habari la IRNA liliripoti. Msemaji wa wizara ya kigeni ya Iran Bahram Qasimi aliitaja ziara hii ya kiongozi wa jeshi la Iran Mohammad Baqri nchini Uturuki na mkutano wake na mwenzake wa Uturuki kuwa ni “muinuko” na “hatua muhimu katika uhusiano baina ya nchi mbili hizi…” (Mehr Iranian Agency 12/8/2017). Kwa hivyo, inatarajiwa sana kuwa ziara hii ilikuwa ni kupanga juu ya kazi yoyote ya kisilaha katika eneo hili, endapo itahitajika ili kufutilia mbali kura ya maamuzi au kuondoa matokeo yoyote yenye kuleta athari… kinachoipatia uzito rai hii ni kule kuzuru kwa Waziri wa Ulinzi wa Amerika Ankara mnamo 23/8/2017 baada ya ziara ya mkuu wa majeshi ya Iran…

D- Ikiwa Amerika itahofia kwamba kwaweza kutokea kwa vurugu kutokana na natija ya nukta (c), Amerika haitazuia kufanyika kwa kura ya maamuzi, lakini bila ya kuwa na matokeo ya maana na yenye athari. Na kwamba kura hii ya maamuzi haitahusisha uchukuaji hatua zozote kwa njia huru.

7. Mwisho, kihakika inaumiza kuona kwamba fungamano la Kiislamu, lililo thaminiwa na Waislamu; Waarabu na Waajemi, makafiri wakoloni wamefaulu kuliweka mbali katika maisha ya Waislamu na kuwabadilishia mafungamano yaliyooza; ya uvunjifu yaliyo wafanya Waislamu kusambaratika: vita baina yao vikikithiri, udugu wao ukitoweka!

Ukabila ni mwiko wa maangamivu kwa Ummah, kama ulivyokuwa jana mwiko wa kuivunja dola ya Kiislamu. Na huyu hapa tena kafir mkoloni anaendelea kuutumia kama silaha kuangamiza kilicho bakia katika nguvu ya Umma ikiwa ataweza… Na kisha kuzigeuza biladi za Waislamu kuwa uwanja wa vita kwa dola kuu na njia ya umwagaji damu za Waislamu, ndugu akikata shingo ya ndugu yake! Uislamu umeharamisha yote haya, na umesisitiza umoja wa Waislamu, na udugu wao, Allah (swt) asema:

**وَاعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا وَاذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنتُمْ أَعْدَاءً فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُم بِنِعْمَتِهِ إِخْوَانًا وَكُنتُمْ عَلَىٰ شَفَا حُفْرَةٍ مِّنَ النَّارِ فَأَنقَذَكُم مِّنْهَا كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ**

**“Na shikamaneni kwa Kamba ya Allah nyote pamoja, wala musifarikiane. Na kumbukeni neema ya Allah iliyo juu yenu: pindi mulipokuwa maadui nyinyi kwa nyinyi basi akaziunganisha nyoyo zenu; mukapambaukiwa hali ya kuwa ni ndugu. Na mulikuwa ukingoni mwa shimo la Moto, naye akakuokoeni nalo. Namna hivi ndivyo Allah anavyo kubainishieni Ishara zake ili mupate kuongoka”.**[Aali Imran: 103].

Na Allah (swt) asema:

**إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ**

**“Hakika ya Waumini ni ndugu”** [Al-Hujurat: 10].

Pia, Uislamu umeharamisha kila aina ya Asabiyah: utaifa, uzalendo na ukabila… nk. Amr ibn Dinar amesema: Nimemsikia Jaber bin Abdullah akisema: tulikuwa pamoja na Mtume (saw) katika vita na mmoja miongoni mwa Muhajirin akampiga mmoja miongoni mwa Maansari. Muansari akapiga ukelele wa kikabila, “Enyi Maansari!” na Muhajir naye akaita, “Enyi Muhajirin!” Mtume wa Allah akayasikia haya akasema, «مَا هَذَا؟» “Ni nini hii?” Wakasema, “Ewe Mtume wa Allah, mmoja miongoni mwa Muhajirin amempiga mmoja miongoni mwa Maansari. Muansari akanadi, “Enyi Maansari!” Na Muhajir akanadi, “Enyi Muhajirin!” Mtume (saw) akasema: **«دَعُوهَا، فَإِنَّهَا مُنْتِنَةٌ»**. “Uacheni, hakika huo ni uvundo”. (Imepokewa na Bukhari).

Na Abi Mijlaz, amepokea kutoka kwa Jundab ibn Abdillah albajali aliyesema: Mtume wa Allah (saw) amesema: **«مَنْ قُتِلَ تَحْتَ رَايَةٍ عُمِّيَّةٍ، يَدْعُو عَصَبِيَّةً، أَوْ يَنْصُرُ عَصَبِيَّةً، فَقِتْلَةٌ جَاهِلِيَّةٌ»** “Yeyote anaye uliwa chini ya bendera ya ukabila, akilingania ukabila, au akiutetea ukabila, basi kifo chake ni cha kijahiliya.” (Muslim).

Waislamu waliishi kwa karne nyingi, wakipata izza kutoka kwa dini yao, wakiwa na nguvu kutoka kwa Mola wao, na kuunganishwa na udugu wao wa Kiislamu. Hivyo basi, miongoni mwa Maswahaba wa Mtume wa Allah (saw) kulikuweko na Abubakar, Omar, Uthman, Ali, Salman al-Farsi (Mfursi) na Bilal al-Habashi (Muhabeshi)… Walikuwa waja wa Allah, ndugu, waliojitolea kwa ajili ya Allah… Kwa hivyo, Omar ambaye ni Muarabu aliingia Al-Qudsi (Jerusalem) kama mkombozi, Salahuddin Mkurdi aliikomboa Al-Qudsi kutoka kwa Makruseda, na Abdulhamid Mturuki aliihifadhi kutokana na uharibifu wa Mayahudi… Kwa hivyo, Waislamu wametukuzwa, na hivyo hivyo kwa kila mwenye moyo, au mwenye kusikia na kutafakari.

**إِنَّ فِي هَٰذَا لَبَلَاغًا لِّقَوْمٍ عَابِدِينَ**

“Hakika katika hii [Qur’an] yapo mawaidha kwa watu wafanyao ibada” [Al-Anbiya: 106]

**18 Dhul Hijjah 1438 H**
**9/9/2017 M**



**Email: uqab@hizb.or.ke**